

## NORTON HEALTHCARE

### Hesabu ya Kiasi Kinachotozwa Kwa Kawaida

Norton Healthcare (pamoja na mashirika yanayohusiana kwa karibu) haitozi wagonjwa wanaostahiki FAP zaidi kwa huduma ya dharura na huduma nyingine muhimu za matibabu kuliko kiasi kinachotozwa kwa kawaida ("AGB") kwa wale amba wana bima inayogharamia huduma hiyo ya matibabu. Badala yake, Norton Healthcare hutoa huduma ya dharura au huduma nyingine muhimu za kiafya bila malipo kwa wagonjwa wowote wanaotimiza vigezo vya kustahiki kwa mpango wa usaizizi wa kifedha chini ya FAP. Norton Healthcare hutumia mbinu ya angalia-nyuma na hukokotoa asilimia ya AGB kwa kila kituo cha hospitali kwa kugawanya jumla ya kiasi cha madai yake ya dharura na huduma nyingine muhimu za kimatibabu ambazo zimeruhusiwa na Medicaid (pamoja na mashirika ya utunzaji yanayosimamiwa na Medicaid na mashirika ya Medicaid yanayohitaji malipo kwa huduma) katika mwaka wa kalenda wa miezi 12 uliotangulia, kwa jumla ya gharama zinazohusiana za madai hayo. AGB inabainishwa kwa kuzidisha gharama za jumla kwa huduma zote zinazotolewa kwa mgonjwa/mdhamini anayestahiki kwenye FAP, ikijumuisha huduma ya dharura na huduma nyingine muhimu za kimatibabu, kwa asilimia ya AGB inayotumika katika jedwali lifuatalo<sup>1</sup>:

Hospitali ya Norton Audubon	18%
<i>Hujumuisha:</i> <i>Kituo cha Matibabu ya Moyo cha Norton - Springs</i>	
Hospitali ya Norton Brownsboro	18%
<i>Hujumuisha:</i> <i>Kituo cha Uchunguzi cha Norton - Dupont</i> <i>Kituo cha Uchunguzi cha Norton - Fern Creek</i> <i>Kituo cha Uchunguzi cha Norton - St. Matthews</i>	
Hospitali ya Norton	20%
Hospitali ya Wanawake na Watoto ya Norton	23%
Hospitali ya Watoto ya Norton	18%
<i>Hujumuisha:</i> <i>Kituo cha Matibabu cha watoto cha Norton</i>	
Hospitali ya Norton King's Daughters' Health	38%
Hospitali ya Norton Clark	25.21%
Hospitali ya Norton Scott	22.77%

---

<sup>1</sup> Utunzaji unaotolewa na Taasisi ya Saratani ya Norton hupewa kituo cha hospitali ambapo kilitolewa na kinaonyeshwa katika asilimia ya AGB ya hospitali hiyo